# UKIUKAJI WA HAKI ZA WATOTO KATIKA RIWAYA YA CHOZI LA HERI

***Dorcas Muendi Musyimi***
*Chuo Kikuu Cha Chuka, Anwani: Box 109-60400, Chuka, Barua Pepe: dmusyimi@chuka.ac.ke*

**How to cite:**
Musyimi, D. M. (2021). Ukiukaji wa haki za watoto katika riwaya ya chozi la heri. In: Isutsa, D. K. (Ed.) *Proceedings of the 7th International Research Conference held in Chuka University from 3rd to 4th December 2020, Chuka, Kenya*, p.429-434

**ABSTRACT**
The aim of this paper is to highlight the abuse of children's rights as portrayed in *Chozi la Heri* (Matei, 2017). It should be noted that a child in this article means both gender; boys and girls. The data for this article was collected through reading the selected text then analyzing it according to the tenets of the Realism Theory as advanced by Ntarangwi (2004) and the article's objectives. The theory applied advances that literature work should portay the world as it is than how it is assumed to be. This paper has depicted that in the *Chozi la Heri* (Matei, 2017) story, children's rights have been abused because there is killing of children, child trafficking, neglect of their health issues, street chidren, child labour, use of chidren in drug trafficking and abuse. In addition, there is girl-child circumcision, lack of parental love and sexual abuse. According to the Realism Theory, this is a true picture of what happens to children in the society. The researcher recommends that children's rights should be respected by every person in the society. These are the future leaders and incase they are affected while young, then there will be a challenge of who to be depended on in the society.
**Keywords**: Rights, Children, Society, Realism.

**IKISIRI**
Lengo la makala haya ni kubainisha ukiukaji wa haki za watoto katika riwaya ya *Chozi la Heri* (Matei, 2017). Ni vyema ikaeleweka kwamba tunapozungumza kuhusu watoto, tunazikusudia jinsia zote mbili. Yaani watoto wa kiume sambamba na wale wa kike. Data ya utafiti huu imepatikana maktabani kwa kusoma riwaya teule kisha ikachanganuliwa kwa misingi ya Nadharia ya Uhalisia kwa mujibu wa Ntarangwi (2004) na lengo la makala. Nadharia hii inasisitiza kuwa kazi za sanaa zinapaswa kujikita katika kuusawiri ulimwengu kama ulivyo wala si kama unavyofikiriwa kuwa. Makala haya yamebainisha kuwa katika riwaya ya *Chozi la Heri* (Matei, 2017) ukiukaji wa haki za watoto upo kwani kuna mauaji ya watoto, ulanguzi wa watoto, kutoshughulikiwa kiafya, kuwepo kwa watoto mitaani, ajira ya watoto, watoto kushiriki katika ulanguzi wa dawa za kulevya na utumiaji wa mihadarati. Isitoshe, imebainika wazi kwamba kuna ukiukaji wa haki za watoto kupitia upashwaji tohara kwa wasichana, ukosefu wa mapenzi ya wazazi na dhuluma za kimapenzi. Kulingana na Nadharia ya Uhalisia, hii ni picha ya yale yanayowatendekea watoto katika jamii ya sasa. Mtafiti anapendekeza kuwa haki za watoto zinahitaji kutiliwa maanani na kila mja yeyote katika jamii. Hawa ndio viongozi wa kesho na iwapo wataathirika wakiwa wachanga basi kutakuwepo na changamoto za adinasi wa kutegemewa katika jamii.
**Istilahi za Muhimu**: Haki, Watoto, Jamii, Uhalisia.

**UTANGULIZI**

Sheria na mikataba mbalimbali inayozungumzia huduma na haki za mtoto, inamtambulisha mtoto kama mtu yeyote mwenye umri wa miaka chini ya 18. Aidha, kwa mujibu wa Hunt (1994) na Sheria ya Mtoto (2010) mtoto ni mwanadamu ambaye hajakomaa kiakili na yuko chini ya miaka kumi na minane. Ni vyema ikaeleweka kwamba tunapozungumza kuhusu watoto, tunazikusudia jinsia zote mbili. Yaani watoto wa kiume sambamba na wale wa kike. Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kunako mwaka 1989 lilipitisha makubaliano ya haki msingi za watoto duniani. Wazo hili limetiliwa maanani na Katiba ya Kenya 2010, sura ya nne sehemu ya tatu, ibara ya hamsini na nne, inayoeleza kuwa watoto wana haki zikiwemo watoto wote, ama waliozaliwa katika ndoa au nje ya ndoa, wako sawa mbele ya sheria na wana haki sawa chini ya Katiba hii. Aidha, maslahi bora ya mtoto yana umuhimu mkubwa katika swala lolote kuhusiana na mtoto. Isitoshe, baba na mamaye mtoto, iwe wameoana au hawajaoana, wana jukumu sawa la kumtunza na kumshughulikia mtoto. Katiba inazidisha kwa kusema kuwa kila mtoto ana haki ya jina na uraia kuanzia anapozaliwa na kusajiliwa kwa kuzaliwa kwake, malezi ya wazazi au yeyote mbadala wakitenganishwa na mtoto ana haki ya elimu ya bure na ya lazima.

Aidha, mtoto ana haki ya kulindwa dhidi ya kubaguliwa, tamaduni za kuumiza, kutumiwa vibaya, kutupwa au kunyanyaswa na kulindwa dhidi ya aina yoyote ya kunyanyaswa na kazi yoyote itakayohatarisha maslahi yao. Kwa kuzidisha, mtoto ana haki ya kupewa chakula cha kutosha, makazi, huduma za malezi ya kiafya na huduma za kijamii. Katiba hii inaoengezea kwa kusema kuwa mtoto ana haki ya kutolazimishiwa ghasia au kuadhibiwa katika njia mbovu, zilizokiuka ubinadamu shuleni na katika taasisi nyingine zinazohusika katika malezi ya watoto. Mtoto hapaswi kushiriki katika uhasama au kujiunga na mizozo ya kutumia silaha badala yake anahitaji kulindwa dhidi ya hali hizo na kutoshikwa au kufungwa isipokuwa endapo hiyo ndiyo hatua ya mwisho. Hili ni dhibitisho tosha kuwa watoto ni sehemu muhimu katika jamii. Makala haya basi yanakusudia kubainisha jinsi mwandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* (Matei, 2017) alivyodhihirisha kukiukwa kwa haki hizi.

**Nadharia ya Utafiti**

Makala haya yametumikiza nadharia ya Uhalisia. Kwa mujibu wa Ntarangwi (2004), nadharia hii katika upana wake, humaanisha uwakilishi wa uhalisi wa mambo katika fasihi. Nadharia hii ilizuka katika karne ya kumi na tisa hususani kwa lengo la kupinga mkondo wa ulimbwende. Mhalisia huamini katika matokeo ya mambo na ukweli anaouzingatia ni ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa kwa tajiriba. Vile vile, wanauhalisia huiamini demokrasia kama hali ya maisha, na malighafi ya kuelezea maisha ya kawaida, ya kadiri na ya kila siku. Hivyo basi uhalisia hujikita katika mambo yaliyopo, tukio mahsusi na matokeo yanayoweza kuthibitika. Imani ya mhalisia ni kwamba kazi ya fasihi yapaswa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida, wa kweli, na halisi. Kutokana na hayo, mhakiki hutazama jinsi ukweli ulivyodhihirishwa katika juhudi za mtunzi za kuchora hali halisi ya mambo katika wakati maalum. Kwa muhtasari makala haya yanakusudia kubainisha jinsi mwandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* (keshatajwa) alivyo wasawiri wahusika, matukio na mandhari yanayokubalika na kuaminika katika jamii ya wakati wake kwa kudhihirisha ukiukaji wa haki za watoto.

**Mbinu za Utafiti**

Data ya utafiti huu ilipatikana kwa kuipitia riwaya ya *Chozi la Heri* (Matei, 2017) na kisha kuichanganua kwa kufuata misingi ya nadharia ya Uhalisia na suala la utafiti.

**Ukiukaji wa Haki za Watoto katika Riwaya ya *Chozi la Heri***

Kutokana na kupitia riwaya husika mtafiti amepata kwamba ukiukaji wa haki za watoto kama zilivyoelezwa katika Katiba ya Kenya (Keshatajwa) umebainika kupitia shughuli zinazofuata.

**Mauaji ya Watoto**

Mwandishi anaelezea jinsi watoto wa Ridhaa ambao ni Tila na Mukeli pamoja na mjukuu wake Becky (uk 5) walivyochomwa katika nyumba kutokana na kutofautiana kwa jamii ya Wahafidhina baada ya wao kuwapigia kura viongozi tofauti. Watoto hawa waliuawa kwani Ridhaa alikuwa akimuunga mkono kiongozi mpya mwanamke-Mwekevu, aliyeshinda badala ya kiongozi mwanamume-Kiboko. Kutokana na mgogoro huu wa kisiasa, mwandishi anasema kwamba kitinda mimba wa Kairu pia alifia mgongoni mwa mamake. Haya yalisababishwa na njaa na ugonjwa wa udhaifu wa mapafu (uk 91).

Maelezo ya mwandishi yanabainisha kuwa mhusika Lemi (uk 120) akiwa miaka 15 alishambuliwa na umati wa watu kwa dai la kuwa mwizi wa rununu. Kitendo hiki kilitendeka alipokuwa ameandamana na dadake-Tindi ili kwenda kununuliwa zawadi ya siku ya kuzaliwa kwake. Tindi aliyekuwa mwanafunzi katika chuo kikuu alijiunga na wengine kusakata densi hadi keshoye bila ufahamu wowote. Njiani wakielekea nyumbani, vurumai ilitokea ambapo mama mpita njia alinyang'anywa simu. Tindi aliamua kukimbia na kumwacha Lemi ambaye umati ulimshuku kuwa mwizi kisha ukamsalimia kwa mawe, tairi kiunoni na kumtia petroli hadi ukamchoma kwa kisingizio tu cha wizi wa rununu ya mama mpita njia. Alikufa kabla ya kufikishwa hospitalini na wasamaria wema.

**Ulanguzi wa Watoto**

Katika riwaya, Umukheri anaelezea jinsi alivyoamka na kujipata yu pweke nyumbani mwao bila nduguze Dick na Mwaliko (uk 82). Dick alikuwa darasa la saba ilhali Mwaliko alikuwa darasa la kwanza. Taswira ya visa vya watoto waliotekwa nyara ilimjia akilini mwake. Ilibidi Umu awaulize majirani ambao hawakuwa na jibu. Hatimaye, alipiga ripoti kwa polisi.

Baadaye iligunduliwa kuwa kijakazi wao Sauna aliyekuwa na mazoea ya kuwateka nyara watoto alikuwa amembadilisha Dick kwa kitita cha pesa ambacho alipewa na Mzee Buda (uk 84). Mwaliko naye alipelekwa kwa Bi Kangara ili wakiisha kuzoeana amuuze.

**Kutoshughulikiwa kiafya**

Mtoto yeyote yule ana haki ya huduma za malezi ya kiafya hata hivyo Kimondo anamwelezea mwanafunzi mwenzake Lunga kuwa siku moja alikuwa na homa ya matumbo (uk 69). Alipomtembelea muuguzi katika kituo cha afya kilichokuwa ndani ya kijiji ambacho mwenye kahawa alikuwa amewajengea wafanyakazi kama babake, daktari alikosa kumtibu kwani alikuwa mtoto wa '*Casual labourer'*.

**Watoto wa Mitaani**

Kulingana na Katiba ya Kenya (keshatajwa), mtoto ana haki ya kupewa makazi. Katika riwaya husika baadhi ya watoto wamo mitaani wakiomba omba kutoka kwa wapita njia. Umu anatupasha kisa cha watoto wa kuombaomba (uk 86) walioishi karibu na kanisa la Mtakatifu Fatma. Kutokana na huruma yake kwao, Umu alimwomba mamake shilingi 20 kisha akaongezea zake mia mbili na kumpa kijana aliyeitwa Hazina. Katika kutembea kwake baada ya Sauna kuwatorosha nduguze; Dick na Mwaliko, Umu alikumbana na kundi kubwa kama wingu la nzige la vijana nje ya mkahawa. Vijana hawa walikuwa na macho mekundu ya kutisha huku wameshika gundi. Alipatana na Hazina akiwa mfanyikazi katika hoteli hii. Hazina alimpeleka katika makao ya watoto alimoishi. Mama Julida aliyekuwa msimamizi wa makao hayo alimpokea Umu (uk 89). Julida alimhakikishia Umu kuwa Wizara ya Elimu ingempa uhamisho kutoka Shule ya Mtende hadi Shule ya Tangamano ambapo angejiunga na kidato cha pili. Katika kisa kingine, Neema bibiye Mwangemi anaelezea jinsi alivyokipata kitoto kimetupwa katika jaa la taka asubuhi moja akielekea kazini (uk 160). Anasema kuwa alikiokota na kukipeleka katika kituo cha polisi. Polisi nao walikipeleka katika kituo cha watoto cha Benefactor. Kitoto kilipokelewa na mtawa Cizarina aliyesema kuwa kitendo cha kuwatupa watoto kilikuwa mazoea kwani mtoto mwingine alikuwa ameachwa langoni mwao huku amefunikwa kijiblanketi kikuukuu. Kitoto hiki kilipewa jina Riziki.

**Ajira ya Watoto**

Msichana Chandachema akiwa katika Shule ya Tangamano anawaelezea wenzake kuwa alipotoka kwa jirani Satua na kumtafuta mamake asimpate, akili yake ilimwelekeza katika kijiji kimoja walikoishi wafanyikazi wa shamba la chai la Shirika la Chai la Tengenea (105). Shamba hili lilimilikiwa na Mzungu mmoja aliyekuwa mlowezi nchini. Chandachema alikimbilia katika shamba hili kwani palikuwa na shule ambayo angejiunga nayo na pia angekidhi mahitaji yake kwa kuchuna majani chai. Alianza masomo katika darasa la pili (uk 105) katika Shule ya Msingi ya Kilimo. Msichana huyu alipokelewa na mwalimu mkuu Bi Tamasha ambaye alimtafutia hifadhi kwa Bwana Tenge na mkewe Kimai (uk 106).

Baada ya miaka mitatu hivi, Chandachema alijiona kama mzigo kwa wahisani wake basi alianza kuchuna majanichai kwa malipo kidogo akiwa darasa la tano. Ilimpasa kurauka alfajiri na mapema ili kuchuna majnichai kabla ya kwenda shuleni saa kumi na mbili asubuhi. Angelala katikati ya michai, kwa marafiki wake, juu ya uchaga mkubwa wa saruji uliotumiwa kama karo na wauza chakula sokoni na wakati mwingine angepita kwa mhisani wake Bwana Tenge (uk 106). Hatimaye Bwana Tenge alihamishwa hadi shamba lingine na Chandachema kuachwa bila makao. Siku ya matokeo ya mtihani wa darasa la nane, mwalimu mkuu alitaka kukutana na mfadhili wake naye Chandachema alimwambia kuwa alikuwa ameacha kuishi na familia ya Bwana Tenge akiwa darasa la sita Bwana Tenge mwenyewe alipopata uhamisho. Bi Tamasha alimtafutia makao katika shirika la Kidini la Hakikisho la Haki na Utulivu (uk 107). Hii ni ishara tosha kuwa haki ya mtoto kulindwa kutokana na kazi yoyote itakayohatarisha maslahi yake imekiukwa kulinganna na mwandishi.

**Ulanguzi wa Dawa za Kulevya**

Mtoto ana haki ya kulindwa dhidi ya kutumiwa vibaya lakini kupitia kwa mwandishi, inabainika kwamba Hazina, kijana aliyewahi kusaidiwa na Umu kwa shilingi mia mbili na ishirini walipopatana kwa mara ya kwanza (uk 88), aliokolewa na serikali kwa kumtoa mtaani alikokuwa akivuta gundi na kutumia mihadarati kisha akapelekwa shule. Walipokutana mara ya pili na Umu, Hazina alikuwa akifanya kazi katika hoteli. Mwandishi anasema kuwa Dick akiwa miaka kumi alikuwa tayari keshalazimishwa kujiunga na biashara haramu ya kuuza dawa za kulevya (uk 119). Kijakazi Sauna ndiye aliyemtosa katika biashara hii. Dick anasema kwamba amesafirisha maelfu na maelfu ya vifurushi vya dawa hizi kwa kuzimeza na kwenda kuzitapika ughaibuni. Sauna alipomwiba Dick, alimpelekea baba tajiri-Mzee Buda aliyejitia kumpeleka shule na badalake alimwigiza katika biashara hii. Kulingana na Selume-muuguzi katika hospitali, Kipanga yumo hospitalini ili kupokea huduma za ushauri nasaha kwani alinusurika kifo kutokana na kangara iliyowaua watu sabini. Vifo hivi vilitokana na unywaji wa pombe (uk 143). Kipanga alianza kunywa pombe akiwa kidato cha pili baada ya kukanwa na aliyemdhania kuwa babake basi akahama alikokuita kwao. Mama mtu alikataa kumwambia nani alikuwa babake.

Kupitia kwa mwandishi, inafahamika kuwa Sauna alikuwa wakala wa Bi Kangara katika biashara ya kulangua watoto (uk 157). Kwa kumtumia Sauna, Bi Kangara aliwapata wasichana wa kuuza katika madanguro na wavulana wa matajiri ili washiriki katika ulanguzi wa dawa za kulevya. Hatimaye, Sauna na Bi Kangara walishikwa na polisi na kushtakiwa kwa ukiukaji wa haki za watoto. Wawili hawa walikuwa wamemweka Mwaliko ambaye alichukuliwa na polisi na kupelekwa katika kituo cha watoto mayatima cha Benefactor (uk 158).

**Upashwaji Tohara**
Watoto wa jinsia ya kike wana haki ya kulindwa dhidi ya tamaduni za kuumiza lakini katika riwaya hii, Tuama yumo hospitalini akihudumiwa na nesi Selume na daktari Meko kutokana na madhara ya tohara (uk 144). Tuama anaelezea kwamba alijipeleka mwenyewe kutahiriwa kwani jamii yake inapendekeza utamaduni huu na kama angekosa wenzake wangemtenga. Tamira aliye dadake Tuama alikuwa ametahiriwa pia.

**Ukosefu wa Mapenzi ya Wazazi**
Mtoto ana haki ya kulelewa na wazazi wawili lakini kitendo hiki ni kinyume na yanayopatikana katika riwaya ya *Chozi la Heri*. Mhusika Selume alipokosana na wakwe zake kutokana na kumuunga mkono kiongozi Mwekevu, aliamua kuondoka na kumwacha mtotoe Sarah mikononi mwa bwanake-Mzee Kaizari (uk 35). Sarah hakupata mapenzi ya mamake. Isitoshe, mwandishi anaelezea kuwa Annette alimnyima Kiriri ushirika wa wanawe kwani alihamia ughaibuni baada ya kupata *Green Card* (uk 64). Watoto wenyewe walipokamilisha masomo yao waliamua kuishi ughaibuni basi wakaendelea kukosa mapenzi ya baba yao. Kutokana na maelezo ya Umu Lunga, familia yao ilihamishwa kutoka Msitu wa Mamba hadi Msitu wa Simba. Wakati huu Umu alikuwa anajiunga na kidato cha kwanza. Serikali iliamua kuwajengea nyumba mpya ambayo haikumpendeza Naomi mamake Umu. Naomi aliamua kuwaacha Umu, Dick na Mwaliko mikononi mwa baba yao Lunga (uk 81). Mwandishi anasema kwamba asubuhi moja Naomi alimwachia Lunga ujumbe mfupi katika rununu na kujiendea zake. Naomi hakuwafahamisha watoto wake juu ya kuondoka kwake. Lunga alilazimika kuwalea watoto wake watatu bila mama mzazi. Baadaye Lunga aligonjeka na kuwaacha watoto wake katika mikono ya kijakazi Sauna. Umu alimlaani mamake kwa kuwatelekeza kwa ubinafsi na ukatili mkuu wa Sauna (uk 84).

Kupitia kwa Kairu inafahamika kuwa maisha yake yalibadilika uongozi mpya uliposhika usukani. Anamwelezea Umu haya wakiwa katika shule ya Tangamano wanakosomea wote wawili kwamba ilibidi familia yao kutoroka. Serikali iliwapa ardhi ya kujengea mabanda. Kairu anasema kuwa alienda pale akiwa darasa la sita na hivi sasa yumo kidato cha pili (uk 92). Anawaelezea wenzake kuwa ana mzazi mmoja tu-mamake aliye muuza samaki. Mapato ya biashara hii hayatoshi kulipia karo ya shule. Kairu aliwahai kumwambia mamake amuulize babake amsaidie kulipa karo lakini mama alimfahamisha kuwa alizaliwa nje ya ndoa basi aliyemdhania kuwa babake alikuwa na familia yake halisi (uk 93). Haya yalimkatisha tamaa.

Msichana Mwanaheri anaelezea kuwa Sarah aliyekuwa mamake alichukiwa na mamkwe kwani alikuwa wa ukoo wa Bamwezi. Mzozo huu ulisababisha mamake kuwatoroka. Asubuhi moja Lime aliyekuwa dadake Mwanaheri aliamka na kupata kibarua juu ya meza ndogo iliyokuwa chumbani mwake. Mama alikuwa amemwacha baba yao Mzee Kaizari na kujiendea zake. Mama alikuwa amemshauri Mwanaheri kumtunza nduguye Lime. Mzee Kaizari alipoamua kumtafuta Sarah alimpata chumbani alikoishi akiwa amekufa kutokana na kunywa sumu. Mwanaheri alijuta kwa kulelewa na mzazi mmoja (uk 95-96).

Mtunzi anasema kuwa Sophie, alilelewa na Apondi baada ya babake Mandu kufia ughaibuni katika shughuli ya kudumisha Amani. Sophie aliachwa na babake akiwa miaka miwili (uk 115) ishara ya kwamba hakuwahi kuyapata mapenzi ya babake hadi alipopangwa na Apondi pamoja na Mwangeka.

**Dhuluma za Kimapenzi**
Watoto wana haki ya kutodhulumiwa kwa vyo vyote vile kimapenzi lakini riwaya hii ina visa vinavyodhihirishwa ukiukaji wa haki hii. Katika riwaya husika, Mzee Kaizari (uk 6) anasema kwamba mabinti wake wawili Lime na Mwanaheri walibakwa na genge la mabarobaro watano. Unyama huu ulitendeka mbele ya macho yake. Mzee Kaizari alijaribu kuwaokoa lakini likawa suala la mume nguvuze. Mabinti hawa waliishi na donda hili. Haya yalikuwa baada ya 'mapinduzi' kumhusu kiongozi mwanamke aliyeitwa Mwekevu ambaye Mzee Kaizari na mkewe Subira walikuwa wakimuunga mkono.

Zohali akiwa katika kidato cha pili alifukuzwa shuleni baada ya kuwa mjamzito (uk 98). Haya yalimtendekea kwa sababu ya papara za ujana. Msichana huyu anawaambia wenzake kuwa amewahi kulala kwenye barabara za jiji pamoja na watoto wengine wa mitaani. Aliwahi kutumia gundi na hata kupigana na majitu yaliyotaka kumnyanyasa kimapenzi. Wenzake mtaani walipoona siku ya kujifungua ikaribu, walimpeleka katika kituo cha Wakfu wa Mama Paulina ambapo alipokelewa na Mtawa Pacha (uk 99). Wazazi wake Zohali walimkana alipohitaji pendo lao. Walimwambia kuwa akishajifungua amtafute babake mtoto ili amsaidie katika malezi. Isitoshe, babake alisisitiza uajiri wa kijakazi na kazi za nyumbani zikamwangukia yeye. Kwa sasa ana mtoto aitwaye Nasibu (uk 101).

Msichana Chandachema anawaambia kina Umu kwamba yeye alikuwa matokeo ya mamake Rehema mwanafunzi wa kidato cha tatu kuringwa na mwalimu wake Fumba (uk 102). Ndoa baina ya Rehema na Fumba ilikataliwa na wazazi ambao walikazania kwamba sharti akamilishe masomo kwanza basi akamkabidhi Chandachema kwa nyanyake ili amlee. Nyanya aliaga Chandachema akiwa darasa la kwanza ndiposa akahamia kwa jiraniye Satua (uk 103). Baada ya miezi miwili Satua alimbadilika Chandachema basi ikambidi atoroke. Alimtafuta mamake asimpate kisha akaamua kutafuta kazi ya kuchuna majanichai katika mashamba ya Shirika la Chai la Tengenea. Shamba hili lilikuwa na Shule ya Msingi ya Kilimo. Alipokelewa na Mwalimu Mkuu Bi.

Tamasha aliyemwahidi kumtafutia hifadhi kwa familia ya Bwana Tenge na mkewe Kimai. Familia hii ilikuwa yenye haja kwani usiku, Chandachema na watoto wao watano walilala mvunguni mwa kitanda cha wazazi. Kulingana na Chandachema, Bi Kimai alipoenda mashambani Bwana Tenge alikibadilisha chumba chao kuwa danguro (uk 106). Angewaleta wanawake mbele ya macho ya wanae hadi usiku wa kuamkia siku ya kurudi kwa Bi Kimai. Watoto walijipata katika dhiki za kisaikolojia ndiposa Chandachema akaamua kuanza kuchuna majanichai kwa malipo kidogo akiwa katika darasa la tano. Hatimaye, Bi Tamasha alimtafutia hifadhi tena katika makao ya watoto mayatima ya Jeshi la Wajane wa Kristu (uk 108).

Mtunzi anarejelea kisa cha Pete ambaye yuko hospitalini. Yeye ni mtoto wa nne katika familia ya watoto sita (uk 146). Alilelewa katika boma la bibi mzaa mamake kwani babake na mamake walikosana basi nyanya akawa ndiye mlezi wake. Katika harakati za kuishi na nyanyake, Pete alipata hedhi akiwa darasa la sita. Hakuwa na uwezo wowote wa kupata sodo ila tambara la blanketi alilopewa na nyanyake. Wiki nzima hakwenda shuleni. Akiwa katika darasa la saba, wajomba wake huku wakiungwa mkono na mamake walipokea posa kisha mahari kutoka kwa mzee Fungo (uk 149). Pete alikuwa amepashwa tohara ishara ya kuwa mkomavu wa kuolewa. Fungo alimwoa kama bibi wa nne. Katika boma hili, Pete alisimangwa na wana wa mke wa kwanza hadi akakichukia kitoto alichokibeba. La mno ni kuwa, aliozwa kwa Mzee Fungo ili jamaa yake ipate pesa za kuwasomesha ndugu zake watano wa kiume. Baada ya miaka minne, Fungo alimfukuza pamoja na mtoto wake. Pete alijitoma katika kampuni ya kutengeneza sare za shule na za wafanyi kazi wa umma. Alihusika na kazi ya kushona vifungo kwenye sare hizi kwa ujira wa shilingi mia mbili kwa siku. Alizitumia kwa mahitaji ya mtoto wake na kodi ya kibanda walimoishi yeye na wenzake wanne. Pia alimlipa msichana mdogo aliyemwajiri kumtazamia kitoto akiwa kazini.

Mhusika Pete anaeleza kuwa akiwa kule kazini alipokea pesa kutoka kwa mibaba iliyodai kukihurumia kitoto chake (uk 151). Kama mwitaji hakuwa na hiari. Mwanamume mmoja aliyeitwa Nyangumi na aliyekuwa ameachana na mkewe, alijitokeza kumpenda kwa dai la kumwoa baadaye. Pete alihamia katika chumba kimoja cha mawe cha Nyangumi. Muungamo huu ulizaa mtoto wa pili. Baadaye, mkewe Nyangumi alimrudia naye Pete akapigwa teke. Huyu wa Nyangumi analelewa na mtoto aliyempata baina yake na Fungo. Pete anasema kuwa alijaribu kukiavya hiki kitoto cha pili mara nne lakini kijusi kikataa. Msichana huyu yuko katika kituo cha afya cha Mwanzo Mpya kwani aliokota kitoto kilicho tumboni katika shughuli ya uuzaji pombe. Anasema kuwa huenda mlevi mmoja alimnyemelea na yakawa haya. Fikira ya kuwa na vitoto vitatu hata kabla ya kufikisha miaka 21 na watoto wa baba tofauti ilimfanya anywe dawa ya panya ili ajiue pamoja na kitoto (uk 152).

Mhusika Sauna akiwa kwa Bi Kangara anakumbuka akiwa kigoli jinsi alivyoamka usiku na kumpata babake kwenye chumba chake cha malazi. Babake, Bwana Maya alimtenda ya kutendwa (uk 154) na baada ya mwezi mmoja alianza kushikwa na kisulisuli, kichefuchefu cha asubuhi nacho kikamwandama. Alipomfahamisha mamake, alipelekwa hospitalini ili kukitungua kile kitoto kabla hakijaumbika. Mamake alimwonya dhidi ya kumwambia yeyote kuhusu unyama wa babake kwani alikuwa amemlea Sauna hata ingawa hakuwa mwana wake wa kumzaa. Sauna aliombwa amsamehe babake kwani hakuna mja aliyekamilika.

Baba yake halisi aliitwa Bwana Kero na mamake alikuwa amemkimbia kabla ya yeye kufa (uk 156). Sauna anasema kuwa hakuwa na matumaini wala hamu ya kuendelea na masomo yake baada ya kuhujumiwa kimapenzi na kihisia. Kitendo hiki kilimfanya kujitoma katika kazi ya machimbo ya mawe na kuuza pombe hadi alipotokea Bi Kangara na kumfundisha biashara ya soko la binadamu. Kazi hii ilimpa pato kubwa (uk 156). Hata hivyo, yeye na Bi Kangara waliishia mikononi mwa polisi na kushtakiwa kwa ukiukaji wa haki za watoto baada ya kugunduliwa.

## HITIMISHO

Kwa ujumla makala haya yamebainisha kuwepo kwa ukiukaji wa haki za watoto katika riwaya ya *Chozi la Heri*. Mtunzi amedhihirisha haya kupitia visa vya mauaji ya watoto, watoto kutoshughulikiwa kiafya, kuwepo kwa watoto mitaani, watoto kushiriki katika ulanguzi wa dawa za kulevya, upashwaji tohara wa wasichana, ukosefu wa mapenzi ya wazazi kwa watoto na dhuluma za kimapenzi. Kupitia katika Nadharia ya Uhalisia ambayo hulenga kuonyesha matukio jinsi yalivyo katika hali ya ukawaida wa wanajamii, hii ni ishara tosha ya uporomokaji wa maadili katika jamii ya sasa. Kulingana na mtafiti, watoto ni sehemu muhimu katika Jamii; basi haki zao zinahitaji kuzingatiwa kwani wao ndio tegemeo la taifa la baadaye katika shughuli za kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa ujumla.

## MAREJELEO


Hunt, P. (1994). *An Introduction to Childrens Literature*. New York. Oxford University Press.

Matei, A. K. (2017). *Chozi la Heri.* Nairobi: One Planet Publishing &Media Services Limited.

Ntarangwi, N. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Augustana College, Rock Island, IL 61201

*The Constitution of Kenya*. (2010). Nairobi: The National Council for Law Reporting. www.kenyalaw.org. Ilichukuliwa 2/9/2020.

*The Children Act*, Revised Edition (2010). Nairobi: The National Council for Law Reporting. www.kenyalaw.org. Ilichukuliwa 2/9/2020.


**********